

SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA NAM.2 YA 2007

MUONGOZO WA MIRATHI YA KIISLAMU

{Chini ya kifungu cha 4 (4)}

VIFUNGU VYA UTANGULIZI

Jina fupi na
kuanza kutumika

1. Muongozo uitajulikana kama Muongozo wa Mirathi ya Kiislamu na utaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Bodi.

Ufafanuzi.

2. Katika Muongozo huu isipokuwa maelezo yakihitaji vyenginevyo:-
"Asaba" maana yake ni kila anaechukua mali yote akiwa peke yake, na anachukua kinachobaki baada ya kupewa warithi wa mafungu.

"Awli" maana yake ni kuzidi kwa asili ya mas-ala na kupelekea kupungua hisa za wenye kurithi kwa mafungu kwa kuzingatia mafungu yao ya asili.

"Baytul mali" maana yake ni mfuko maalum ulioanzishwa kwa ajili ya kuhifadhi mali za waislamu na kuzitumia kwa maslahi ya Uislamu na waislamu.

"Babu sahihi" maana yake ni babu anaehusiana na marehemu kwa upande wa kwa baba tu na inakusanya babaake baba, babaake babaake baba na kupanda juu kwa kutaja mababa watupu.

"Bibi Sahihi" maana yake ni bibi anaehusiana na marehemu kwa upande wa kwa mama na inakusanya mamaake mama, mamaake mamaake mama na kupanda juu kwa kutaja mamama watupu; Aidha, bibi anaehusiana na marehemu kwa upande wa kwa baba na inakusanya mamaake baba, mamaake mamaake baba.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya uongozi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar.

“Dhawil Arham” maana yake ni kila jamaa wa karibu, mwenye uhusiano wa damu na marehemu na akawa hayumo miongoni mwa warithi wa mafungu wala uasaba.

“Fungu” maana yake ni kiwango maalum kilichokadiriwa na kupangwa na Mwenyezi Mungu kwa mrithi ndani ya tirka.

“Kamisheni” maana yake ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar.

“Katibu Mtendaji” maana yake ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na mali ya Amana au anefanya majukumu yake kisheria.

“Khuntha Mushkel” maana yake ni mtu ambae ana ala ya uzazi ya mwanamme na mwanamke kwa pamoja; au hana ala yoyote; na ikawa haijabainika kama ni mwanamme au mwanamke.

“Kuhujubu” maana yake ni kuzuiliwa mrithi asirithi katika tirka yote au kupunguziwa kwa kuwepo mwenye haki zaidi ya kurithi kuliko yeye.

“Mahkama” maana yake ni Mahkama Kuu ya Zanzibar, Mahkama ya Kadhi au mahkama nyengine yoyote iliyochini ya Mahkama Kuu.

“Maradhi ya mauti” maana yake ni maradhi ambayo yanampata mwanadamu na akawa hatarajiwi kupoa.

“Mas-ala” maana yake ni hesabu ya mirathi.

“Mirathi” maana yake ni kuondoka umiliki kutoka kwa mtu aliekufa kwenda kwa warithi wake waliokuwa hai sawa kama kilichowachwa ni mali au haki miongoni mwa haki za kisheria.

“Mrithi” maana yake ni mtu aliye hai kiuhakika au kwa hukumu ambaye imemthibitikia sababu miongoni mwa sababu za mirathi.

“Mrithiwa” maana yake ni mtu aliyefariki kiuhakika au kwa hukumu na akawacha mali au haki za kimali ambazo zinapaswa kuondoshewa umiliki wake kwenda kwa wanaomstahikia.

“Mtoto” maana yake ni Mwana anaetambulika katika sheria ya Kiislamu sawa awe mwanamme au mwanamke, wa umri wowote atakaokuwa, pia inakusanya mtoto wake (mjukuu) wa mtoto mwaname na mtoto wa mtoto wake mwanamme na kushuka chini zaidi.

“Mwenye kuzuiliwa kisheria” maana yake ni Mtu aliyezuiliwa na Mahkama yoyote yenye mamlaka kufanya matumizi yoyote katika mali yake kutokana na sababu mbali mbali kama vile ufujaji wa mali, ubadhirifu, kukopa sana, kudaiwa sana au sababu yoyote kama itakavyoona Mahkama.

“Radd” maana yake ni kupungua asili ya mas-ala na kupelekea kuzidishiwa wenye kurithi kwa mafungu zaidi ya hisa zao kwa kuzingatia mafungu yao ya asili.

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana namba 2 ya mwaka 2007 na marekebisho yake.

“Tirka” maana yake ni kile anachokiwacha mtu baada ya kifo chake katika mali, haki za kimali na haki zisizo zisizo za kimali.

“Wasia” maana yake ni kumilikisha mali au haki ambapo utekelezaji wake unianza baada ya kufa mtoa wasia.

“Waziri” maana yake ni Waziri anayesimamia Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana.

Matumizi

3. Bila ya kuathiri matakwa ya Sheria, Kamisheni katika kutekeleza majukumu yake itazingatia misingi ya Muongozo.

Haki zilizoshikamana na Tirka

4. Tirka imeshikamana na haki zinazotekelezwa kwa utaratibu ufuatao:

(1)-Kulipwa gharama za mazishi bila ya kuchupa mpaka tokea kufa kwake hadi kutiwa kaburini.

(2)-Kulipwa madeni sawa kama:-

(a) Yamefungamana na dhima ya marehemu au mali yake.

(b) Madeni ya Mwenyezi Mungu au ya watu.

(3)-Kutekelezwa wasia.

(4)-Kugaiwa warithi kilichobaki katika tirka kwa mujibu wa Shariah na kanuni hizi.

VIFUNGU VYA WASIA

Utekelezaji Wasia

5. (1) Wasia utatekelezwa baada ya kutolewa gharama za mazishi na kulipwa madeni ya marehemu.

(2)(a) Ili wasia utekelezwe itapaswa usizidi thuluthi na usiwe kwa Warithi.

(b) Iwapo wasia ukizidi thuluthi na ukiwa miongoni mwa warithi Utekelezaji wake utategemea ridhaa ya warithi.

(c) Iwapo baadhi ya warithi watakataa na wengine kukubali utekelezaji wake utakatwa kutoka katika mafungu ya waliokubali tu.

(d) Mazingatio ya kuwa alieusiwa ni mrathi au sio mrathi yatategemea kama atapata fungu katika mirathi wakati wa kurithisha.

6. Wasia wowote wenye masharti, utatekelezwa iwapo tu masharti hayo hayapingani na sheria, sharia za Kiislamu au Muongozo huu.

Matumizi katika maradhi ya mauti

7. Maagizo ya kumilikisha mali au haki yatakayotolewa na mtu wakati wa maradhi ya mauti yatachukuliwa kuwa ni wasia.

Nguzo za wasia

8. Wasia uliokamilika una nguzo zifuatazo:-

(1) Tamko ambalo linakusanya kuandika na lugha za alama kwa asiyeweza

kutamka.

(2) Mtoaji wasia ni lazima awe balebeghe mwenye akili timamu na awe hajazuliwa na sheria.

(3) Mpewaji wasia

(4) Kinachousiwa ambacho ni lazima kiwe ni milki ya mtoaji na ni cha halali.

Kubadilisha wasia
na kughairi

9. (1) Inaruhusiwa kwa mtoaji wasia, kubadili au kughairi katika wasia wake ikiwa ni wote au sehemu yake tu.

(2) Matumizi ya mtoaji wasia katika mali au haki aliyoitolea wasia kunachukuliwa kuwa ni kughairi katika wasia

Kusikilizwa madai
ya wasia na
kuthibitisha kwake

10. (1) Madai ya wasia au kughairi katika wasia hakutathibiti ila kwa ushahidi wa maandishi rasmi.

(2) Madai yoyote ya wasia au kughairi yasiyokuwa ya maandishi rasmi yatapaswa kuthibitishwa kwanza na Mahkama isipokuwa yakiridhiwa na Warithi wote na ridhaa hiyo kuidhinishwa na Katibu Mtendaji.

Sharti za kusihi
wasia kwa upande
wa mpewaji wasia

11. Ili wasia uwe sahihi kwa upande wa mpewaji wasia ni lazima:-

(1) Awe yupo wakati wa kutolewa wasia, na kwamba uwepo huo uwe ni wa hakika, au hukumu au kukadiria.

(2) Asiwe ni muuaji wa mtoaji wasia kwa namna yoyote itakayothibitishwa kisheria.

(3) Isiwe ni taasisi ya maasi kwa mujibu wa Shariah za Kiislamu.

(4) Kuukubali wasia baada ya kufa muusiaji sawa kama ni binafsi, wakala au walii wake. Kukaa kimya kunahesabika kuwa ni kuukubali wasia.

Kutofautiana dini
na uraia

12. Ikiwa anayeusiwa ametofautiana dini au uraia na mwenye kuusia, Wasia huo utasihi na kutekelezwa.

Kunyang'nyiana
wasia

13. Ikiwa wasia ni zaidi ya thuluthi kwa watu zaidi ya mmoja, na warithi hawakuridhia kuzidisha zaidi ya thuluthi inayokubalika kisheria basi itagawiwa thuluthi hiyo kwa waliousiwa kwa kupunguzwa kwa mujibu wa

asilimia za hisa za thamani ya vitu walivyoukiwa.

Wasia
usioteketezeka au
uliokataliwa

14. Iwapo wasia haukutekelezeka kwa namna yoyote ile au ukikataliwa na mpewaji utarejeshwa katika tirka.

VIFUNGU VYA MIRATHI

Nguzo za Mirathi

15. Ili mirathi itimie ni lazima ziwepo nguzo zifuatazo:

- (1) Mrithiwa. Nae ni mtu aliekufa kwa hakika au kwa hukumu.
- (2) Mrithi. Nae ni mtu aliehai wakati wa kifo cha mrithiwa na zikawepo sababu za kurithi.
- (3) Tirka nayo ni mali au haki inayorithiwa.

Sababu za mirathi

16. Sababu zinazompelekea mtu kumrithi marehemu ni:-

- (1) Udugu wa damu kinasabu.
- (2) Ndoa iliyo sahihi hata kama haikupatikana dukhuli.
 - (a) Mke aliyeachwa Talaka Rejea ana haki ya kurithi na kurithiwa ndani ya kipindi cha eda.
 - (b) Mke aliyeachwa talaka ya tatu katika maradhi ya mauti ana haki ya kumrithi mumewe, lakini mume hana haki hiyo.
- (3) Baytul mali ya Waislamu.

17. Iwapo Mrathi anahusiana na marehemu kwa sababu zaidi ya moja basi atarithi kwa kuzingatia sababu zote bila ya sababu moja kuathiri nyengine. Kwa mfano ni mume lakini pia ni mtoto wa Ami.

Sharti za Mirathi

18. Ili mirathi ifanyike ni lazima masharti yafuatayo yakamilike:

- (1) Kufariki mtu anayerithiwa kwa hakika au hukumu ya Mahkama.
- (2) Kuhakikika uhai wa mrithi wakati wa kufa anayerithiwa.
- (3) Kufahamika pande zinazostahiki kurithi.

Vizuizi vya Mirathi

19. Mambo yafuatayo yatamzuwilia mtu kurithi hata kama anastahiki kurithi:

- (1) Kuuu sawa kama ni kwa kukusudia au bila kukusudia.
- (2) Kutofautiana dini wakati wa kufa anaerithiwa. Muislamu harithiani na mpagani au mfuasi wa dini, Itikadi au Madhehebu yoyote yaliyokuwa nje ya Uislamu.

20. Mtu anapozuiliwa mirathi kwa kizuizi chochote kati ya vilivyotajwa katika Kanuni ya 19 ya kanuni hizi atahesabika kuwa hayupo kabisa kabisa hivyo hatoweza kuleta athari yoyote katika mirathi.

Kufa kwa watu wawili au zaidi kwa pamoja

21. Wakifa watu wawili au zaidi ambao wanarithiana na ikawa haikujulikana aliyekufa mwanzo kati yao, au alijulikana akasahaulika basi hakuna yeyote miongoni mwao mwenye haki ya kurithi katika tirka ya mwenziwe.

Daraja za Warithi

22. Katika kurithisha kunafuatwa utaratibu maalumu wa ngazi. Haishukwi daraja nyengine ila wanapokosekana walio katika daraja hiyo au wanapopewa mirathi yao na ikabakia. Utaratibu huo ni kama ufuatao:-

- (a) Kuwagawia wanaorithi kwa mafungu.
- (b) Kuwagawia wanaorithi kwa uasaba
- (c) Kurudishwa kilichobaki kwa warithi wa mafungu isipokuwa mume na mke.
- (d) Kuwarithisha *Dhawil Arham*.
- (e) Kurudishwa kilichobaki kwa mume au mke.
- (f) Kupewa aliyeusiwa kwa zaidi ya thuluthi moja iwapo anazo sifa za kutekelezewa wasia.
- (g) Kupelekwa *Baitul Mali*.

Wanaostahiki kurithi

23.(1) Jumla ya watu wanaostahiki kurithi ni 23. Kati yao wanaume ni 14 na Wanawake ni tisa. Kwa urefu orodha yao imebainishwa katika Jadueli Namba "A" la Muongozo huu.

(2) Wapo warithi wanaorithi kwa mafungu maalum tu, wapo wanaorithi Kinachobakia tu na wapo wanaorithi kwa mafungu na kinachobakia.

Warithi wa Mafungu Maalum

24(1) Mafungu maalumu yanayotumika kugawa tirka ni saba. Mafungu hayo

ni nusu ($\frac{1}{2}$), Robo ($\frac{1}{4}$), Thumuni ($\frac{1}{8}$), Thuluthi ($\frac{1}{3}$), Thuluthi mbili ($\frac{2}{3}$), Sudusi ($\frac{1}{6}$) na Thuluthi ya kilichobaki ($\frac{1}{3}$ ya B).

(2) Warithi wanaorithi kwa mafungu maalum ni kumi na moja nao ni:

- (a) Mume.
- (b) Mke.
- (c) Mtoto mwanamke
- (d) Mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme
- (e) Dada khalisa.
- (f) Dada wa baba moja.
- (g) Ndugu wa mama mmoja mwanamme au mwanamke.
- (h) Mama.
- (i) Baba.
- (j) Babu sahihi.
- (k) Bibi sahihi.

(3) Ufafanuzi wa mafungu wanayostahiki kurithi na sharti za kurithi kwao zimefafanuliwa katika Jaduweli namba "B" la Muongozo huu.

(4) Pindi ikiwa mke au bibi wapo zaidi ya mmoja basi litagaiwa fungu lao sawa sawa kati ya wake au mabibi hao.

Mas-alatu
Omariyyatayni

25. (1). Mas-alatul Omariyyatayni au Gharawayni ni mas-ala ambayo marehemu amewacha baba, mama pamoja na mke au mume.

(2) Katika mas-ala hii mama atachukua thuluthi ya kinachobakia baada ya kutolewa fungu la mume au mke.

(3) Anapokuwepo babu pahala pa baba, mama atachukua thuluthi ya tirka yote.

Mas-ala
Kushirikiana.

26. Ikiwa katika tirka wapo warithi wa mafungu, ndugu wa kwa mama na kaka khalisa au kaka pamoja na dada khalisa; na warithi wa mafungu pamoja na ndugu wa kwa mama wakaimaliza tirka yote bila ya kubakisha kitu kwa Asaba ambao ni ndugu khalisa; basi ndugu khalisa watachukuliwa kama ni ndugu wa kwa mama na watashirikiana na ndugu wa kwa mama katika thuluthi kwa kugawana sawasawa na bila kubaguwa kati ya wanaume na wanawake.

Mirathi ya Asaba 27. (1) Mirathi ya Asaba inakuwa kwa utaratibu, hivyo mwenye haki zaidi ndie anaechukua mali yote au kilichobaki baada ya warithi wa mafungu. Iwapo hakikubakia kitu baada ya kupewa warithi wa mafungu basi Asaba atakosa isipokuwa katika mas-ala ya kushirikiana iliyotajwa katika kifungu cha 26 cha Muongozo huu.

(2) Watashirikiana Maasaba katika kustahiki sehemu yao ya mirathi wakiwa katika kundi, daraja na nguvu zilizo sawa; na mwanamme atachukua sawa na wanawake wawili wakiwa ni wanawake na wanaume walio katika kundi, daraja na nguvu sawa.

Aina za Asaba 28. Wako Asaba wa aina tatu kama ifuatavyo:

(1) Asaba kwa Nafsi yake. Mara nyingi linapotamkwa neno Asaba tu huwa linakusudiwa kundi hili.

(2) Asaba kwa Mwengine.

(3) Asaba pamoja na mwengine.

Asaba kwa Nafsi yake 29. (1) Nae ni mrithi mwanamme ambae haingii katika kunasibiana kwake na marehemu mrithi mwanamke. Aina hii inakusanya mtoto mwanamme, mtoto mwanamme wa mtoto mwanamme (*na kushuka chini*), baba, babu babaake baba (*na kupanda juu*), kaka khalisa, kaka wa kwa baba, mtoto mwanamme wa kaka khalisa (*na kushuka chini*), mtoto mwanamme wa kaka wa kwa baba (*na kushuka chini*), Ami khalisa (*na kupanda juu*), Ami wa kwa baba na (*kupanda juu*), Mtoto mwanamme wa Ami khalisa (*na kushuka chini*) na Mtoto mwanamme wa Ami wa kwa baba (*na kushuka chini*).

(2). Wanapokusanyika maasaba kwa nafsi zao wengi katika tirka moja, basi unatangelizwa upande wa Utoto wenye watoto na wajukuu; asha Ubaba wenye baba na mababu; kIsha Ukaka wenye makaka na watoto wao; na mwisho Uami wenye maami na watoto wao.

(3) Wanapokusanyika babu na kaka khalisa au wa kwa baba hapo watashirikiana katika kurithi kama ilivyobainishwa katika kifungu cha

32 na 33 vya Muongozo huu. Hata hivyo mirathi hiyo haitowahusu watoto wa ndugu.

(4). Wanapokusanyika maasaba wengi wa upande mmoja, hutangulizwa aliye daraja ya juu ambayo iko karibu zaidi na marehemu. Inakusudiwa watoto kabla ya wajukuu, baba kabla ya babu, kaka kabla ya watoto wa kaka na ami kabla ya watoto wa ami.

(5) Wanapokusanyika maasaba wengi wa daraja moja, wanatangulizwa wenye nguvu zaidi ya ujamaa mfano kaka khalisa kabla ya kaka wa kwa baba.

Asaba kwa Mwengine 30. Asaba kwa mwengine ni kila mrithi mwanamke mwenye fungu anapounganishwa na kaka yake aliye Asaba kwa nafsi yake. Aina hii ya Asaba inakusanya mtoto mwanamke kwa kuwepo mtoto mwanamme, mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme kwa kuwepo mtoto mwanamme wa mtoto mwanamme, dada khalisa kwa kuwepo kaka khalisa na dada wa kwa baba kwa kuwepo kaka wa kwa baba.

Asaba pamoja na Mwengine 31. (1) Asaba pamoja na mwengine ni kila mrithi mwanamke mwenye fungu katika upande wa undugu akikutana na mrithi mwanamke katika upande wa utoto. Aina hii ya Asaba inakusanya dada khalisa au dada wa kwa baba akiwa pamoja na mtoto mwanamke au mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme.

(2)Asaba pamoja na mwengine anakuwa na nguvu za kurithi sawa na kaka yake anapokuwa Asaba kwa nafsi yake katika kuwazuilia maasaba walio katika upande, daraja au nguvu za chini zaidi.

Mirathi ya Babu na Ndugu khalisa au wa kwa baba tu 32.(1) Iwapo Babu anarithi na ndugu khalisa tu au wa kwa baba tu sawa kama ni wanaume watupu, wanawake watupu au mchanganyiko na hayupo pamoja nao mwenye kurithi kwa mafungu basi babu atapewa kilicho bora kwake kati ya:-

(a) thuluthi ya Tirka; au

(b) Kugawana na ndugu kwa utaratibu wa mwanamme kuchukua sawa na wanawake wawili.

(2) Iwapo yupo mwenye kurithi kwa mafungu, basi huchukua mwenye kurithi kwa mafungu kwanza kisha:-

(a) Ikihakikwa sudusi atachukua babu.

(b) Ikihakikwa kasoro kuliko sudusi itafanywa iwe sudusi na atapewa babu na mas-ala itakuwa na *awli*.

(c) Katika hali zilizotajwa kwenye vifungu 32(2) (a) na (b) ndugu wataanguka na hawatorithi kitu.

(d) Iwapo imebaki zaidi ya sudusi ya Tirka, babu atapewa kilicho bora zaidi kwake kati ya sudusi ya Tirka, thuluthi ya kilichobaki au kugawana na ndugu kilichobaki.

Mirathi ya Babu na ndugu khalisa na wa ndugu wa kwa baba kwa pamoja

33 (1) Wakijumuika ndugu khalisa na wa kwa baba pamoja na babu, ndugu wote hushirikiana kupunguza fungu la babu katika kugawana kisha watakorithi fungu la ndugu ni ndugu khalisa tu kwa utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 32.

(2) Hawarithi ndugu wa kwa baba ikiwa yupo babu na ndugu khalisa isipokuwa awe ndugu khalisa ni mwanamke mmoja tu na iwe baada ya kupata babu imebakia zaidi ya nusu ya Tirka.

Mas-alamatul Akdariyya

34. Ikiwa katika tirka wapo mume, mama, babu na dada khalisa; warithi wote watachukua mafungu yao kisha babu atachanganya fungu lake la sudusi pamoja na fungu la dada khalisa la nusu na watagawana dada na babu kwa utaratibu wa mwanamme kupata sawa na wanawake wawili.

Kuhujubiana

35. (1) Mrithi aliyehujubiwa harithi chochote katika tirka au hupata fungu dogo kwa kuwepo mwenye haki zaidi kisheria. Hata hivyo aliyehujubiwa kuwepo kwake kuna athari katika mirathi. Hivyo, kuwepo kwa ndugu wengi waliohujubiwa kunapunguza mirathi ya mama anaparithi na baba kutoka thuluthi kwenda sudusi.

(2) Ufafanuzi wa wanaohujubiwa na warithi wanaowahujubu umetolewa katika Jaduweli namba "C" la Muongozo huu.

Mirathi Radd yenye

36.(1) Ikiwa wanaorithi kwa mafungu hawakuimaliza tirka na hakuna Asaba yeyote; basi kitarejeshwa kilichobaki kwa watu wa mafungu kulingana na

mafungu yao isipokuwa mume au mke.

(2) Ikiwa hakuna mrithi yeyote kati ya wanaorithi kwa mafungu, Asaba wala *Dhawil – Arham* isipokuwa mume au mke, basi kitarejeshwa kilichobaki kwa mume au mke.

Mirathi yenye Awli. 37. (1) Ikiwa wanaorithi kwa mafungu hisa zao zitaizidi asili ya mas-ala, basi hali hiyo itapunguza kiwango cha mafungu yao waliyostahiki kurithi.

(2) Kitazingatiwa kile kilichozidi ndio Asli ya Mas-ala na itagaiwa tirka kwa mujibu wa Asili hiyo.

Mirathi ya Dhawil Arham 38. (1) Katika kurithisha Jamaa wa karibu utatumika utaratibu wa *Ahlu tanzil*.
(2) Chini ya Utaratibu huo, itaangaliwa asili anayotokea jamaa wa karibu miongoni mwa warithi wa mafungu na uasaba na atapewa sehemu ambayo angestahiki huyo mrathi wa asili kama angekuwepo mwenyewe. Mfano mtoto wa dada khalisa atarithi mirathi ya dada khalisa.

Mirathi ya mtu aliyepotea. 39.(1) Mtu anapopotea na/au ikiwa hakuna mawasiliano yoyote; itakadiriwa kuwa yuko hai na litatolewa na kuzuliwa fungu lake katika tirka. Iwapo atatokea atapewa fungu lake alilorithishwa.

(2)Iwapo itathibitika kuwa amekufa au akihukumu Kadhi kuwa amekufa:

(a) Iwapo kifo hicho ni kabla ya maiti wa mwanzo basi mirathi itafanywa upya na aliyepotea atazingatiwa kuwa hayupo. Hivyo, fungu lake lililozuliwa watapewa warithi wengine wa tirka hiyo.

(b) Iwapo itathibiti kuwa amekufa baada ya maiti wa mwanzo, basi fungu lililozuliwa watarithishwa warithi wa aliyepotea.

(3) Iwapo aliyepotea itahukumiwa kuwa amefariki, kisha akatokezea yuko hai hali ya kuwa fungu au tirka yake imeshagawiwa; basi atakuwa na haki ya kukichukua atakachokikuta mikononi mwa warithi katika mali yake na hatorejeshewa wala kudai kilichokwisha kutumika.

Mirathi ya Mimba 40. (1) Mimba itastahiki kurithi iwapo itakuwa imeshatunga katika tumbo la mama yake wakati wa kifo cha anaerithiwa; na iwapo itazaliwa mtoto akiwa hai japo kwa kulia tu.

(2) Mimba inaweza kuzaliwa mtoto mmoja au wengi, wanaume, wanawake au mchanganyiko hivyo mirathi ya mimba itafanywa kama ifuatavyo:-

(a) Iwapo mimba haitorithi kwa hali yoyote basi mirathi hugawiwa bila ya kusubiriwa au kuzingatiwa mimba.

(b) Iwapo mimba inarithi lakini katika baadhi ya hali ina fungu kubwa zaidi kuliko nyengine litazuiliwa fungu lililokuwa kubwa zaidi na kilichobaki watarithishwa warithi wengine kwa mujibu wa haki zao.

(c) Iwapo hakuna mrithi zaidi ya mimba au warithi waliopo wanaweza kuhujubiwa katika baadhi ya hali za mtoto basi mali yote itazuiliwa mpaka izaliwe mimba.

(3) Baada ya mimba kuzaliwa, mali iliyozuiliwa itagawiwa kwa mujibu wa taratibu na kama yupo mrithi aliyepunguziwa atarejeshewa haki yake kutokana na kilichozuiliwa.

Mirathi ya Khuntha
Mushkeli

41. Iwapo katika warithi yumo khuntha mushkeli, basi mas-ala itafanywa mara mbili; kwa kuzingatia kuwa khuntha huyo ni mwanamme na nyengine mwanamme. Kisha kila mrithi akiwemo khuntha atapewa kilicho kichache kwa sababu ndio kilichothibiti kwa yakini na kitakachobaki kitazuiliwa mpaka itakapobainika jinsi ya khuntha.

Mirathi ya
walioghariki au
kufa kwa pamoja

42. (1) Iwapo watu wanaorithiana watakufa kwa pamoja kwa ajali au tukio lolote na ikajulikana aliyetangulia kukata roho japo kwa muda mfupi sana, basi aliyekufa mwisho atamrithi aliyekufa mwanzo.

(2) Iwapo haitojulikana aliyekata roho mwanzo basi hawatorithiana wote na watahesabiwa kuwa hawapo katika tirka ya kila mmoja kwa mwenzake.

Mirathi yenye kesi
ya Mrithi, Mali au
Wasia

43. (1) Iwapo Mirathi ina kesi inayohusu Mrithi au wasia na baadhi ya warathi wakataka mirathi hiyo igawiwe, basi mas-ala itafanywa mara mbili; kwa kuzingatia kushinda kwa pande mbili zinazopingana. Kisha kila mrithi atapewa kilicho kichache kwa sababu ndio kilichothibiti kwa yakini na kitakachobaki kitazuiliwa mpaka itakapotoka hukumu ya kesi na kumalizika muda wa rufaa.

(2) Iwapo kesi ya Mirathi itahusu umiliki wa mali, mirathi itaendeshwa kwa mali zisizo na kesi tu na mali yenye kesi itasubiri mpaka itakapotoka hukumu

ya kesi na kumalizika muda wa rufaa.

Mirathi
kutumia
madhehebu
nyengine
Kiislamu

kwa 44. (1) Iwapo warithi wote kwa kauli moja watataka kurithishwa kwa fik-hi ya madhehebu nyenginezo za Kiislamu miongoni mwa madhehebu zinazotumika za hapa Zanzibar watalazimika kumuandika Katibu Mtendaji ombi lililosainiwa na warithi wote wakieleza sababu na madhehebu wanayotaka yatumike katika kurithisha tirka yao.

(2) Kamisheni ikiridhia kutumia madhehebu mengine katika kurithisha mirathi iliyotajwa katika Kifungu kidogo cha (1) sawa kama ni kwa masharti au bila ya masharti; inaweza kuomba usaidizi kutoka kwa mwanachuoni wa madhehebu husika ambae atabainishwa kama rejea ya mas-ala hiyo mahsusi.

(3) Kukihitajika gharama zozote za ziada katika kufanikisha mirathi ya aina hii zitalipwa na warithi.

TARATIBU ZA USIMAMIZI WA KIOFISI

Ufunguzi
Mirathi

wa 45. Kutakuwa na aina tatu za ufunguzi wa Mirathi katika Kamisheni kama ifuatavyo:-

(1) Kamisheni kupokea tirka kutoka Serikalini, taasisi ya umma au binafsi au mtu mwingine yeyote kwa lengo la kurithishwa.

(2) Mrithi au mtu mwingine yeyote kuleta fomu ya Mirathi iliyojazwa na kusainiwa na Sheha wa eneo lake au Mkuu wa Wilaya.

(3) Kamisheni kufungua mirathi yenyewe kwa nguvu iliyopewa na Sheria

Usajili, kuchukuwa
maelezo, vielelezo
na kumbukumbu

46. Mara tu baada ya kufunguliwa mirathi na kuwekwa jalada maalum, Kamisheni itaisajili Mirathi hiyo na kuipa namba kisha itachukua hatua zifuatazo:-

(1) Itawataka warithi au wasimamizi kuwasilisha vielelezo vya marehemu, warithi au Tirka kama itavyoona inahitajika.

(2) Itawaita wahasika wote wa mirathi hiyo au wawakilishi wao ili kuthibitisha warithi, tirka, wasia, madeni na taarifa zote zinazohusia na

mirathi hiyo.

(a) Maelezo yoyote atakayoyotoa mrithi au mtu yeyote anaehusika yataandikwa kisha mhusika atasomewa na akiyaridhia atatia saina yake na tarehe.

(b) Nyaraka, kumbukumbu, mawasiliano na taarifa zote zinazohusu mirathi iliyosajiliwa na kupewa namba maalum zitahifadhiwa Kamisheni katika jalada lake linalohusiana na tirka ya marehemu.

Jalada dogo

47. (1) Hairuhusiwi kwa tirka yoyote kufunguliwa jalada dogo (sub-file) la tirka hiyo ila kwa idhini ya maandishi ya Katibu Mtendaji.

(2) Katika kuomba idhini ya kufungua jalada dogo, Afisa Urithi ataeleza sababu za kutaka kufanya hivyo na ataandika maelezo ya kina na taarifa muhimu za jalada la asili.

Vipaumbele katika kurithisha

48. (1) Mali yenye kuhamishika haitakuwa na kipaumbele juu ya warithi wote ambapo kila mmoja atapewa haki yake.

(2) Mali isiyohamishika itakuwa na kipaumbele katika kumilikishwa kisheria kwa utaratibu ufuatao:-

(a) watoto wa marehemu.

(b) wazee wa marehemu.

(c) mke au mume wa marehemu.

(d) hawashi ambao ni ndugu na watoto wao, maami, makaka na warithi wengineo wa marehemu.

Kuendelea na mirathi hata kama hawakupatikana wahusika wote

49. Bila ya kuathiri Kifungu kidogo cha (2) cha Kifungu cha 46 cha Muongozo huu mhusika yeyote atakapoitwa mara mbili na Kamisheni ili kutoa taarifa zake na akawa hakuhudhuria, hakuwasilisha taarifa zake, wala kutoa taarifa ya udhuru wake kimaandishi kwa Kamisheni atahesabika kuwa anawafikiana na maamuzi yote yatakayotolewa na Kamisheni.

(1) Kutokuhudhuria au kukataa kutoa ushirikiano kwa Mrithi yeyote hakutoizuwia Kamisheni kuendelea na hatua za kurithisha.

(2) Mtu au Taasisi inapoizuwia Kamisheni kufanya wajibu wake wa Kurithisha kwa kuficha taarifa au kutokutoa ushirikiano inaoombwa katika kuiwezesha Kamisheni kufikia kutoa uamuzi wa haki inaweza kuchukuliwa hatua kama ilivyotajwa katika Sheria.

Mizozo na Utata
wakati wa
kurithisha

50. (1) Mzozo au utata wowote utakaotokea kutokana na warithi, tirka, wasia, madeni au taarifa yoyote utasuluhishwa na Kamisheni na sulhu isipofikiwa; Kamisheni itatoa maamuzi na Mhusika asieridhika na uamuzi huo, anaweza kufungua dai la kupinga Mahkamani.

(2) Mhusika asieridhika na uamuzi wa Kamisheni atatakiwa kumuarifu Katibu Mtendaji kuhusu nia yake ya kwenda mahkamani si zaidi ya wiki mbili tokea uamuzi huo ulipotolewa; na baada ya kupokea taarifa Kamisheni itatoa muda usiozidi siku thelathini za kalenda ili kumuwezesha kukamilisha taratibu za kufungua dai hilo Mahkamani.

(3) Muda huo utakapomaliza bila ya dai hilo kufunguliwa Mahkamani, wala kuletwa sababu au hoja zitakazoikinaisha Kamisheni kutengua maamuzi yake au kutoa muda wa ziada basi Kamisheni itatekeleza maamuzi iliyoyafikia.

(4) Kanuni hii haihusiani na kadhia ya uhalali wa mrithi iliyotajwa katika kifungu cha 62(1) cha Sheria.

Kuhakiki,
kutathmini
kurithisha mali

51. (1) Kamisheni itazifuatilia mali za tirka, itazitathmini na kuzirithisha kama itakavyokubaliana na warithi.

(2) Kamisheni itazigawa miongoni mwa warithi mali halisi zilizomo katika Tirka sawa kama ni zenye kuhamishika au zisizohamishika kwa kuzingatia vipaumbele vya warathi vilivyotajwa katika Kifungu cha 48.

(3) Iwapo mali hizo hazigawiki kwa asili yake au kutokana na mzozo wa warithi, Kamisheni itazitia thamani mali husika kupitia sehemu zenye utaalumu na kuwataka warithi wafidiane kwa kuzingatia thamani hiyo, wingi wa haki zao na vipaumbele; na iwapo hautopatikana muwafaka kuhusiana na bei au mnunuzi, basi mali husika zitauzwa kwa mnada wa hadhara na mrithi yeyote atakaezitaka mali anaweza kuingia katika mnada.

(4) Bila ya kuathiri Kifungu kidogo cha (3) cha Muongozo huu, mrithi asieridhika na uamuzi wa Kamisheni wa kuiuza mali kwa mnada atalazimika kupinga uamuzi huo mahakamani kwa kufuata hatua zifuatazo:-

(a) Kuiaifu Kamisheni kwa maandishi kuwa atapinga uamuzi huo Mahkamani ndani ya wiki mbili baada ya uamuzi huo kutolewa.

(b) Kamisheni itatoa siku thelathini za kalenda baada ya kupokea idhari hiyo bila ya kutekeleza maamuzi ya kuuza kwa mnada; na iwapo siku hizo thelathini zitapita bila ya kufunguliwa dai hilo, wala kutolewa sababu au hoja zitakazoikinaisha Kamisheni kuongeza muda au kutengua uamuzi wake basi itaendelea na hatua za mauzo kwa mnada.

Kufunga Hesabu
ya Mirtahi

52. (1) Baada ya kukamilika taratibu zote, Kamisheni itafunga hisabu ya mirathi kwa mujibu wa Shariah ya Kiislamu, Sheria na Muongozo huu.

(2) Mas-ala ya mirathi inaweza kufungwa kwa kila marehemu kama ni kesi inayojitegemea au kwa njia ya *munasakhaati*, baada ya mashauriano baina ya wahusika na Kamisheni; katika kuamua hili uamuzi wa Kamisheni utakuwa ndio wa mwisho.

(3) Hisabu ya mirathi itahesabika kuwa imeshafungwa na tayari kwa kulipwa au kutolewa hati baada ya kupitiwa, kusahihishwa na kutiwa saini na watu wafuatao:-

(a) Afisa wa Urithi aliyeifunga hisabu hiyo.

(b) Mkuu wa Urithi, Msaidizi Mkuu wa Urithi au Afisa aliyeidhinishwa kufanya kazi zao.

(c) Mchunguzi wa ndani, Msahihisha hesabu au Afisa aliyeidhinishwa kufanya uchunguzi.

(d) Mhasibu Mkuu au Msaidizi Mhasibu Mkuu au Afisa aliyeidhinishwa.

(e) Katibu Mtendaji au Afisa aliyeidhinishwa kufanya kazi zake.

(f) Mtu mwengine yeyote ambae Katibu Mtendaji ataelekeza kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli hizi.

Wajibu

wa 53. (1) Afisa wa Urithi atahakikisha usahihi na ukamilifu wa majina ya

wasahihishaji

wahusika wa mirathi, umri, mali, urithi, vielelezo, viambatanisho, maelezo, mawasiliano na mpangilio wake katika jalada.

(2) Mkuu wa Urithi atathibitisha maelezo ya Afisa wa Urithi.

(3) Mchunguzi wa ndani atahakikisha usahihi na ukamilifu wa fedha na thamani ya mali zilizorikodiwa, zilizoingia, malipo, haki na ada zilizotoka, vielelezo vya hesabu na malipo, uwiano wa jalada na rekodi nyenginezo, usahihi wa hesabu, kinacholipwa na wanaolipwa.

(4) Mhasibu Mkuu atalipitia jalada na hesabu na kuangalia taratibu za fedha na malipo na akiridhika atapendekeza kwa Katibu Mtendaji kufanyiwa malipo urithi huo.

(5) Katibu Mtendaji atalipitia jalada lote na akiridhika, ataidhinisha mgao wa tirka hiyo.

Kitangulizi
Malipo cha

54 (1) Mrithi yeyote ambaye tirka yake inaendeshwa na Kamisheni na tayari mali au haki hiyo imeshakabidhiwa na imo katika udhibiti wa Kamisheni, anaweza kuomba kwa maandishi kitangulizi cha malipo ya sehemu ya haki yake kwa Katibu Mtendaji ambae akiridhika anaweza kuidhinisha malipo hayo.

(2) Kabla ya kufanywa malipo ya kitangulizi, Afisa Urithi anayehusika ataandaa rasimu ya mgao wa urithi huo na baadae rasimu hiyo itapitia katika taratibu za kawaida za urithishaji.

Hati ya Uwakala

55.(1) Hairuhusiwa kwa mtu yeyote kumuwakilisha mwengine katika taratibu za urithi isipokuwa kwanza awe na Hati ya Uwakala (power of attorney) iliyotolewa katika vyombo vya kisheria na iwe imetimia kwa mujibu wa sheria za nchi husika.

(2) Kifungu kidogo cha (1) cha Muongozo huu hakiwahusu watoto wadogo wala wale wasiokamilika utu wao.

(3) Bila ya kuathiri matakwa ya Sheria, Haki ya mtoto au mtu asiekamilika utu ikiwa si yenye thamani kubwa anaweza kupewa mama, baba au yeyote

alie na dhamana ya mtu huyo baada ya kupatikana ridhaa ya Katibu Mtendaji.

(4) Kamisheni inaweza kuandaa Hati ya Kiapo au uthibitisho mwingine utakaotumika ikiwa itakubaliwa na wahusika wote waliopo na kuridhiwa na Katibu Mtendaji.

Barua
Usimamizi
mirathi.

ya
wa

56. (1) Mtu yeyote aliyepatiwa na Mahkama Barua ya Usimamizi wa Mirathi kwa idhini ya Kamisheni, atalazimika kuwasilisha Kamisheni muhtasari wa hatua alizochukua na hesabu ya Mgao.

(2) Msimamizi atakayerithisha bila ya kufuata utaratibu wa Sheria na wa Kanuni hizi atakuwa ni mkosa na urithishaji wake hautokuwa halali isipokuwa ukithibitishwa usahihi wake na Katibu Mtendaji.

(3) Hati ya Usimamizi wa Mirathi haitatolewa isipokuwa kwa Tirka inayohitaji ufuatiliaji nje ya Zanzibar, uwakilishi katika Mahkama au sababu nyengine itatakayoridhiwa na Bodi.

Kubadilisha jina

57. Pale ambapo Kamisheni itarithisha mali inayohamishika kama vile gari, jukumu la kubadilisha jina litakuwa ni la mrithi mwenyewe kwa mujibu wa sheria nyenginezo za nchi, isipokuwa Kamisheni itamrahisishia mrithi huyo kwa kumpatia uthibitisho wa umiliki wa mali hiyo baada ya kurithishwa.

MAKOSA MBALIMBALI NA ADHABU ZAKE

Makosa na Adhabu
zake

58. Mtu yeyote ambaye:-

- (a) atakwenda kinyume na matakwa ya Kanuni hizi
- (b) ataitumia, ataihodhi, ataizua, ataingia, ataivamia tirka yoyote;
- (c) ataweka kikwazo, atakataa kuitikia wito, au ataizua kwa njia yoyote Kamisheni au maafisa wake kutekeleza kazi na majukumu yao kuhusiana na tirka yoyote;
- (d) atamchochea, atamshawishi mtu mwingine kufanya jambo lililokatazwa au kutokufanya jambo lililoamrisha na Sheria au Muongozo huu;

Atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani ataswa kulipa faini isiyozidi shilingi

milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili kwa pamoja kwa mujibu wa kifungu cha sheria Nam.2 ya mwaka 2007.

MENGINEYO

Fomu na Nyaraka
mbalimbali

59. Katika kutekeleza kazi zake, Kamisheni itatumia karatasi, fomu na nyaraka mbalimbali.

JADUWELI "A"
WANAOSTAHIKI KURITHI

	WANAUME		WANAWAKE
1	Mtoto mwanamme	1	Mtoto mwanamke
2	Mtoto mwanamme wa mtoto mwanamme (<i>na kushuka chini</i>).	2	Mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme (<i>na kushuka chini</i>)
3	Baba	3	Mama
4	Babu baba ake baba (<i>na kupanda juu</i>)	4	Bibi mzaa mama
5	Ndugu mwanamme khalisa	5	Bibi mzaa baba
6	Ndugu mwanamme wa kwa baba	6	Ndugu mwanamke khalisa
7	Ndugu mwanamke wa kwa mama	7	Ndugu mwanamke wa kwa baba
8	Mtoto mwanamme wa ndugu mwanamme khalisa (<i>na kushuka chini</i>)	8	Ndugu mwanamke wa kwa mama
9	Mtoto mwanamme wa ndugu mwanamme wa kwa baba (<i>na kushuka chini</i>)	9	Mke
10	Ami khalisa (<i>na kupanda juu</i>)		
11	Ami wa kwa baba (<i>na kupanda juu</i>)		
12	Mtoto mwanamme wa Ami khalisa (<i>na kushuka chini</i>)		
13	Mtoto wa mwaname wa Ami wa kwa baba (<i>na kushuka chini</i>)		
14	Mume		

JADUWELI "B"
WARITHI WA MAFUNGU, VIWANGO VYAO NA MASHARTI YA KUSTAHIKI

	MRATHI	FUNGU	SHARTI ZA KURITHI
a.	Mume	Nusu (1/2)	Asiwepo mtoto wala mjukuu mwenye kurithi
		Robo (1/4)	Akiwepo mtoto au mjukuu mwenye kurithi
b.	Mke/ Wake	Robo (1/4)	Asiwepo mtoto wala mjukuu.
		Thumuni (1/8)	Akiwepo mtoto au mjukuu.
c.	Mtoto mwanamke	Nusu (1/2)	a. Asiwepo mtoto mwanamme <i>muasibu</i> (atakaemfanya awe Asaba). b. Awe peke yake (mmoja tu).
		Thuluthi mbili (2/3)	a. Asiwepo mtoto mwanamme muasibu. b. Wawe wengi (kuanzia wawili).
d.	Mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme	Nusu (1/2)	a. Asiwepo mjukuu wa kiume muasibu b. Awe peke yake (mmoja tu). c. Asiwepo mtoto.
		Thuluthi mbili (2/3)	a. Asiwepo mjukuu wa kiume muasibu b. Wawe wengi (zaidi ya mmoja). c. Asiwepo mtoto .
		Sudusi (1/6)	a. Akiwepo mtoto wa kike mmoja anaerithi 1/2. b. Asiwe mjukuu wa kiume muasibu. (wakiwa wengi pia watagawana sudusi hii).

e.	Ndugu mwanamke khalisa	Nusu (1/2)	a.Asiwepo kaka khalisa muasibu. b.Awe peke yake. c.Asiwepo <i>mzazi wa kiume</i> (baba au babu). d. Asiwepo mtoto wala mjukuu
		Thuluthi mbili (2/3)	a.Asiwepo kaka khalisa muasibu. b. Wawe wengi. c. Asiwepo mzazi wa kiume. d. Asiwepo mtoto wala mjukuu
f.	Ndugu mwanamke wa kwa baba	Nusu (1/2)	a.Asiwepo kaka wa kwa baba muasibu. b.Awe peke yake. c. Asiwepo mzazi wa kiume. d. Asiwepo mtoto wala mjukuu e. Asiwepo ndugu Khalisa
		Thuluthi mbili (2/3)	a.Asiwepo kaka wa kwa baba muasibu. b. Wawe wengi. c. Asiwepo mzazi wa kiume. d. Asiwepo mtoto wala mjukuu e. Asiwepo ndugu khalisa.
		Sudusi (1/6)	a.Akiwepo dada khalisa mmoja anaerithi 1/2. b.Asiwepo kaka wa kwa baba muasibu. (wakiwa wengi pia watagawana sudusi hii).
g.	Ndugu wa kwa mama	Thuluthi (1/3)	a.Asiwepo mzazi wa kiume (baba au babu). b. Asiwepo mtoto wala mjukuu. c. Wawe zaidi ya mmoja (wanawake, wanaume au kwa pamoja).
		Sudusi (1/6)	a.Asiwepo mzazi wa kiume (baba au babu). b. Asiwepo mtoto wala mjukuu. c. Awe mmoja pekee.
. h.	Mama	Thuluthi (1/3)	a.Asiwepo mtoto wala mjukuu. b.Wasiwepo ndugu zaidi ya mmoja sawa kama ni khalisa, wababa, wa mama au mchanganyiko. c. Isiwe katika masalatul Omariyyatayni.
		Sudusi (1/6)	a.Akiwepo mtoto au mjukuu. b. Akiwepo ndugu zaidi ya mmoja.
		Thuluthi ya baki (1/3 B)	Katika mas-alatul Omariyyatayni. (Anaporithi mama pamoja na baba na mke au mume).
i.	Baba	Sudusi (1/6)	Iwapo yupo mtoto au mjukuu
j.	Babu alie sahihi	Sudusi (1/6)	a.Akiwepo mtoto au mjukuu . b.Asiwepo baba.
k.	Bibi alie sahihi	Sudusi (1/6)	a.Asiwepo mama. b. Asiwepo baba (ikiwa ni bibi mzaa baba).

JADUWELI "C"
KUHUJUBIANA (KUZUILIANA KURITHI)

ANAEZUIWA	ANAEZUIA
1. Mjukuu wa kiume	Mtoto wa kiume, mjukuu wa karibu wa kiume atamzuia mjukuu wa mbali.
2. Mjukuu wa kike	Mtoto wa kiume, watoto wanawake wawili na zaidi isipokuwa akiwepo Muasibu,
3. Babu	Baba, babu wa karibu.
4. Bibi mzaa mama	Mama au bibi wa karibu ikiwa daraja yake ni mama mkubwa.
5. Bibi mzaa baba	Mama, baba, bibi wa karibu ikiwa daraja yake ni mama mkubwa.
6-7. Kaka/dada khalisa	Mtoto wa kiume, mjukuu wa kiume, baba.
8-9. Kaka/dada baba mmoja	Mtoto wa kiume, mjukuu wa kiume, baba, dada khalisa pindipo akiwa ASABA pamoja na mwengine.
10-11. Kaka/dada mama mmoja	Mtoto wa kiume au kike, mjukuu wa kike au kiume, baba na babu.
12-13. Mtoto wakiume wa kaka khalisa	Mtoto wa kiume au kike, mjukuu wa kiume au kike, baba, babu, kaka khalisa, kaka baba mmoja
14-15 Mtoto wa kiume wa kaka baba mmoja	Mtoto wa kiume/kike, mjukuu, wa kiume/kike baba, babu, kaka khalisa, kaka baba mmoja, mtoto wa kiume wa kaka khalisa.
16. Ami khalisa	Mtoto au/na mjukuu wakiume, baba, babu, kaka khalisa kaka baba mmoja, mtoto wa kiume wa kaka khalisa mtoto wakiume wa kaka baba mmoja.
17. Ami baba mmoja	Mtoto au/na mjukuu wa kiume, baba, babu, kaka khalisa au/na baba mmoja, mtoto wa kiume wa kaka khalisa au/na baba mmoja, ami khalisa.
18. Mtoto wa kiume wa ami khalisa	Mtoto/mjukuu wa kiume, baba, babu, kaka khalisa/baba mmoja, mtoto wa kiume wa kaka khalisa/baba mmoja ami khalisa, ami baba mmoja.
19. Mtoto wa kiume wa ami baba mmoja	Mtoto/mjukuu wa kiume, baba, babu, kaka khalisa/baba mmoja mtoto wa kiume wa kaka khalisa/baba mmoja ami khalisa ami baba mmoja, mtoto wa kiume wa ami khalisa.

